

IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 4

Novemba 2022

# HABARINJEMA KILA SIKU KWA WATOTO

FREE

HAKIUZWI

KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI KISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25

Uebert & BeBe ANGEL



## UEBERT & BEBE ANGEL

Waanzilishi wa Ubalozi wa Kiroho (Kanisa la Habari Njema)Ulimwenguni, Manabii' Uebert na Bebe Angel wanayo furaha kuleta kwako Habari Njema ya kila siku wa Watoto.
Kila siku neno la Mungu linafurahisha! Tumehakikisha kila somo ni rahisi kulisoma na kuelewa.

Watoto watafarijika watakapo soma na kutamka Tamko la kinabii kwenye maisha yao kilasiku. Ujumbe huu pia una wavutia Watoto wadogo kuwa na wakati wao maalumu wa utulivu wa kujisomea "Somo zaidi" na kujiwekea notsi za jinsi walivyo elewa kwenye dayari zao. Mizizi ya imani ya mkristo itaendeshwa kwa undani zaidi kwenye mioyo yao kadiri wanavyo kua kiroho na kuelewa Habari Njema ya neema ya Mungu katika umri mdogo.

# My goodnews notes



**Matendo 6:15**
**"Watu wote kwenye ule mkutano walikuwa wanamtazama Stefano Kwa makini. Uso wake ukaonekana kama uso wa malaika."**

Kwani unajua kama ukisali Kwa kunena Kwa lugha, sura yako inabadilika? Kwenye kioo unaweza kuonekana ivyo hivyo, lakini wengine wanakuona umebadilika.

Andiko letu la leo linamuongelea Stefano, mtu aliyetumiwa na Mungu sana. Wale wakubwa wanapomkamata Stefano na kumpeleka mahakamani, kila mtu alimuangalia na sura yake ilikuwa kama sura ya malaika. Kitu gani kilitokea? Stefano alikuwa mtu wa kuomba. Aliongea na Mungu kila kitu kinachotokea kwenye maisha yake na maisha ya watu wengine. Alikuwa akiomba kwaajili yake na wengine, pamoja na majirani, kazini kwake, na kuombea mji. Unapofanya hivi tena na tena, sura yako, sauti yako, na kila kitu kinachokuhusu wewe kinabadilika. Utaanza kuongea neno la Mungu kwa kujiamini.

Leo unaposali, omba kwaajili ya familia yako, majirani, na hata nchi yako, na alafu utaona unavyobadilika kama Stefano.

## TAMKO LA KINABII

**Mimi ninaleta mabadiliko, Ninageuza vitu vinavyonizunguka kupitia maombi. Ninapoomba, familia yangu, shule, mjini na nchi yangu vinabadilika na kuwa vizuri zaidi na zaidi katika Jina la YESU. Amina!**

**SOMO ZAIDI**
Matendo 6:8-15



**Luka 18:1**
**"Akawaambia kwa mfano, imewapasa kumwomba Mungu siku zote na wala wasikate tamaa."**

Wakati mtoto Penguini anazaliwa,mama yake anabaki na kumlinda mtoto wakati baba anaenda baharini kuwinda chakula. Pengwini wanakaa kwa makundi makubwa yanayoitwa koloni, kundi linakuwa na mamia na ma elfu ya pengwini wanaofanana. Kwa hiyo baba anaporejea, anaenda kumtafuta mke wake na mtoto pengwini kwenye kundi kubwa lenye kelele la koloni! Anafanya hivyo Kwa njia gani?

Anasikiliza sauti ya kipekee ya mke wake na mtoto pengwini na kuzifuata. Huifuata sauti mpaka anawapata na kuwalisha. Kama mke au mtoto pengwini wakikaa kimya hawawezi kupata chakula chao au kumuona baba tena.

Kuna kelele nyingi duniani za mabilioni ya watu wakilia kama koloni za pengwini, lakini Mungu husikiliza tu sauti za maombi kutoka kwa watoto wake.

Kamwe usiache kuomba ili sauti yako kila wakati isikike, na hautokata tamaa.

## TAMKO LA KINABII

**Asante Roho mtakatifu kwa kunisaidia kuomba.Ninapo omba leo, Ninajua Bwana amenisikia na amenijibu maombi yangu katika Jina la YESU.**

**SOMO ZAIDI:** 1 Yohana 5:15



HABARI NJEMA KILA SIKU KWA WATOTO



**1 Timotheo 2:1**
**"Kwanza, Ninawaambia ombeni kwaajili ya watu wote. Waombeeni watu vitu wanavyohitaji kwa Mungu, na muwe watu wa kumshuru."**

Bahari inamwambia nini Nahodha wa Meli? Haisemi kitu! Bahari yenyewe inarusha tu mawimbi. Habari Njema kwako mtoto wa Mungu. Je wajua ni nini Nahodha anafanya kwenye Meli? Yeye Kazi yake ni kuhakikisha abiria wake na mizigo yao wako salama.

Unapokuwa Mkristo, unakuwa pia Nahodha. Unakuwa Nahodha wa familia yako, shule yako, na majirani zako. Hii maana yake, kama Nahodha tu wa kawaida, unahakikisha wako salama wale wanao kuzunguka na unawaombea. Angalia andiko letu la leo: Waombeeni watu vitu wanavyohitaji kwa Mungu. Hautoweza kujua nini rafiki zako, familia, au shule wana hitaji, lakini unaponena kwa lugha ya Roho mtakatifu, unaomba Sawa Sawa Mungu anachotaka wapate, na utaona mabadiliko.
Haleluya!

Kuanzia leo, tumia muda kuwaombea wengine.

## TAMKO LA KINABII

**Kama Nahodha wa kizazi, Ninaombea familia yangu, shule yangu, majirani na Mataifa. Ombi langu linasababisha mabadiliko katika jina lenye nguvu la Yesu! Amina.**

**SOMO ZAIDI**
1 Timotheo 2:1-3



1 Yohana 5:14
"Tunaweza kuja kwa Mungu bila kuwa na mashaka. Hii humaanisha kwamba tunapomuomba Mungu vitu (na vitu hivyo kama vinaendana na kile anachotaka Mungu kwetu), ndiposa Mungu huzingatia kile tunachosema."

Je, umewahi kujaribu kumuomba mtu kitu ambacho hana? Kwa mfano, fikiria unamuomba rafiki yako mbwa, lakini rafiki yako hana mbwa. Waweza tu kuomba kama unajua mtu anacho unachokiomba, si ndiyo?

Ni hivyo pia kwa Mungu.Unapomuomba kitu, inabidi iwe ni kitu ambacho unajua anacho. Utajua vipi kama Mungu anacho unachokiomba? Ni kwa kutafuta kwenye mistari ya Biblia inayoongelea kile unachokitaka .Kwa mfano, Ikiwa unamuomba Mungu akusaidie kufanya kazi ngumu ya shuleni uliyopewa kufanya nyumbani, tazama mstari unaoongelea kuhusu hekima. Kwa mfano, Mungu ni hekima yetu (1 Wakorintho 1:30 ICB), Na anampatia kila mtu. Unapopata mstari huu wa biblia, sasa unapoomba, unatamka tena huo mstari kwa Mungu. Hivyo ndio Kuomba Neno.

Na chochote unachokiona kigumu, tafuta mstari wa biblia unaozungumzia hicho kitu na ukiombe.

## TAMKO LA KINABII

**Ninaomba neno, na Bwana hunisikiliza kila mara. Maisha yangu ni ya kushangaza katika jina la Yesu!**

**SOMO ZAIDI:** 1 Yohana 5:14-15



**Ufunuo 1:6**
**"Alitufanya kuwa ufalme wa makuhani wenye kumtumikia Mungu Baba yake. Kwake Yesu Kristo uwe utukufu na nguvu Milele na milele!Amina."**

Yaani, Nampenda Yesu! Unafahamu anachofanya kuhani?Katika nyakati za zamani, watu hawakuweza kuzungumza na Mungu kama tunavyofanya sasa. Mungu aliongea na watu maalumu tu kama makuhani, Na makuhani walirudisha ujumbe kwa watu.

Lakini sasa umefanyika kuwa kuhani! Utukufu kwa Mungu! Hii inamaanisha kwamba Mungu husikiliza kila neno unalolitamka. Unaona, Kuhani kamwe hasemi maneno mabaya kuhusu yeye au wengine. Unapozungumza maneno mazuri, Mungu anasikia na kutenda maneno yako.

Kuanzia leo, zungumza maneno mazuri tu kuhusu wewe na wengine na utazame jinsi maisha yako yatabadilika kuwa bora.

## TAMKO LA KINABII

**Ninazungumza kama kuhani leo, na kila kitu katika maisha yangu kinabadilika kuwa bora katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI**
Marko 11:23



**Yohana 6:63**
**"Siyo mwili wenye kumpa mtu uzima. Ni roho ndio huleta uzima. Maneno niliyowaambia ni roho, na hivyo yanaleta uzima."**

Je! Umewahi kutazama katuni ambapo kuna mwana mazingaombwe? Mwana mazingaombwe anasema "abrakadabra", na mara sungura hutokeza. Sasa basi, neno "abrakadabra" maana yake ninatamka, na kinakuwa halisi. Wana mazingaombwe wanatumia ujanja mwingi kuwafanya watu wafikiri kuwa sungura katokea tu hewani. Lakini wewe una kitu halisi na bora zaidi.

Andiko letu la leo linasema maneno tunayoongea ni roho na yanaleta uzima. Chochote unachosema kinafanyika kuwa kitu halisi. Kama ukijitamkia mabaya mwenyewe ukisema, "Mimi sio mwerevu" au "Siwezi kufanya" hiki au kile, basi itakuwa hivyo. Lakini ukijisemea vizuri, "Mimi ni mwerevu", Ninaweza kufanya mambo yote katika Kristo Yesu", "Mimi ni mwanafunzi bora darasani". Hata kama haujihisi hivyo, inakuwa halisi. Tenda Sawa Sawa na Mungu anavyotenda na kusema vitu ambavyo havipo kama vile vipo!

Kamwe usisikilize maneno mabaya yanayosemwa juu ya maisha yako; Ongea vizuri tu kuhusu wewe mwenyewe.

## TAMKO LA KINABII

**Ninavyozungumza, inakuwa halisi kwasababu maneno ninayoongea ni roho na yanaleta uzima. Haleluya!**

**SOMO ZAIDI :** Warumi 4:16



HABARI NJEMA KILA SIKU KWA WATOTO



**Mathayo 5:14**
**“Wewe ni Nuru iletayo mwanga duniani. Mji uliojengwa juu ya mlima hauwezi kufichika.”**

Watoto, andiko letu la leo linasema wewe ni mji! Ni miji mingapi unaweza kuitaja? Kuna London, New York, Harare, Sydney, Mumbai, na kuendelea. Miji huwapatia watu mahitaji yote wanayohitaji ili waishi. Katika miji kuna Benki, Shule, hospitali, maduka ya chakula, na ofisi za polisi ambazo huwalinda raia dhidi ya watu wabaya.

Sasa Mungu anakuita wewe Mji pia kwa sababu, ndani yako unacho kilakitu ambacho mji unavyo! Fikiria kuhusu hili: wewe mwenyewe ni hospitali maana una afya ya Mungu; Unaye Roho mtakatifu anayekufundisha kila kitu, kwahiyo wewe mwenyewe ni shule! Si ajabu Ibrahimu aliitwa baba wa mataifa mengi.

Wiki hii tutajifunza zaidi kuhusu kujenga mji wetu kwa kutumia neno la Mungu.

## TAMKO LA KINABII

Mimi ni mji uliojengwa juu ya mlima na haufichiki. Ninakopesha mataifa na kamwe sita pungukiwa chochote katika Jina la Yesu!

**SOMO ZAIDI**
Mwanzo 17:5



**Warumi 8:11**
**"Mungu alimfufua Yesu kutoka kifo. Na kama Roho wa Mungu anaishi ndani yako, basi atawapatia pia uzima kwenye miili yenu inayokufa. Mungu ndiye aliyemfufua Kristo kutoka kwenye kifo. Naye atawapa uzima kupitia Roho wake Mtakatifu anayeishi ndani yenu."**

Watoto, kwanini daktari alikasirika sana? Kwasababu aliishiwa wagonjwa!Tunaongelea wewe ukiwa kama Mji. Mji wa kawaida unayo hospitali, si ndiyo? Sasa basi, Ninaenda kukuonyesha kuwa unayo hospitali bora zaidi ndani yako.

Ni nini mbaya kuliko kuwa mgonjwa? Inauma sana. Lakini angalia andiko letu linasemaje leo, unaye Roho yule yule aliyemfufua Yesu kutoka kwenye kifo! Kama unaye uyo huyo Roho aliyemfufua Yesu kutoka katika kifo, basi Roho uyo huyo atahakikisha unadumu katika afya mfululizo! Roho mtakatifu anakupa uzima ambao Mungu anao, yeye ambaye kamwe hawezi kuumwa. Wasisitize watu unaowajua wanaougua Kumpokea Kristo na wataponywa kama vile wameenda hospitali. Jenga Mji wako pamoja na hospitali yako kwa kuutamkia afya mwili wako Kila siku.

## TAMKO LA KINABII

**Ninakiri na kutamka kwamba Roho yule yule aliyemfufua Yesu kutoka kwenye kifo anaishi ndani yangu. Nimebeba afya ya Mungu na kamwe sitougua! Amina!**

**SOMO ZAIDI:** Mathayo 15:30



**Yohana 14:26**
**"Lakini msaidizi atawafundisha kila kitu. Atafanya mkumbuke vitu vyote nilivyowaambia. Huyu msaidizi ni Roho Mtakatifu ambaye Baba atamtuma kwa jina langu."**

Watoto, ni kwanini macho ya mwalimu yaliduwaa? Hakuweza kuwadhibiti wanafunzi wake!

Hivi unajua unayo shule yako ndani yako? Mstari wetu wa leo unatuambia kwamba Roho Mtakatifu ni mwalimu wetu na anatufundisha kila kitu. Kila kitu ni vitu vingapi? Ni kilakitu, ni vitu vyote!Kwahiyo, kama unahitaji msaada wa kufanya kazi yako ya shuleni, kazi nyumbani au kuielewa Biblia, Atakufundisha kila kitu. Unachotakiwa kufanya ni kumuambia. Ni Msaidizi wako na anapenda kushirikishwa Kwenye kila kitu kidogo unachofanya. Shuleni, unao walimu wa masomo tofauti, lakini katika shule yako, mwalimu wako Roho Mtakatifu anajua kila somo. Utukufu!

Jenga shule ya Mji wako kwa kutamka kwamba Roho mtakatifu ni mwalimu wako na umuambia akusaidie somo lolote.

## TAMKO LA KINABII

**Roho Mtakatifu ni msaada wangu, na ananifundisha vitu vyote. Majibu yote ninayo hitaji yapo ndani yangu katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI**
Zaburi 46:1



**Warumi 8:17**
**"na kama watoto, basi warithi wa Mungu na warithi pamoja na Kristo,..."**

Watoto, Nisaidieni kwanza hili. Ni wapi samaki wanaweka pesa zao? Kwenye benki ya maji!Utaelewa hii ukifika nyumbani. Bado tunajenga mji wako, na leo nataka nikuonyeshe unayo benki yako mwenyewe ndani yako.

Pengine umewahi kuwaona watu wanaenda benki. Hawa watu wanaenda benki au kwenye mashine kuchukua pesa wanapo hitaji. Lakini unajua kama mwana wa Mungu, pesa zako hazipo benki? Unazo pesa nyingi zaidi unavyofikiria! Andiko letu linatuambia kwamba sisi ni warithi wa Mungu, Mrithi ni mtu anayemiliki kila kitu ambacho Baba au Mama yake wameacha kabla ya kuondoka duniani. Mungu anamiliki pesa zote duniani, na hizo zote ni zako! Kwahiyo, wakati wewe na familia yako mnahitaji pesa, unachotakiwa kufanya ni kuijenga benki ya Mji wako tamka neno la Mungu na useme "PESA ZINAKUJA!" kilasiku na uangalie Mungu akiwapa. Utukufu!

## TAMKO LA KINABII

**Ninakiri na kutamka pesa zinakuja! Haziletwi na benki Bali Mungu. Haleluya!**

**SOMO ZAIDI**
Zaburi 112:3



**2 Wafalme 6:17**
**"Basi Elisha aliomba,"Bwana,fungua macho ya mtumwa wangu. Muache aone."Bwana akayafunua macho ya kijana mdogo.Na akaona kuwa mlima umejaa farasi na magari ya vita yenye moto kumzunguka Elisha."**

Mji wowote una Jeshi au polisi kukamata waalifu. Wewe pia unalo jeshi la polisi ndani yako. Kwenye mstari hapo juu, Nabii Elisha alikuwa amezungukwa na maadui, lakini alikuwa na jeshi lake mwenyewe ambalo maadui hawawezi kuliona.Mlima ulijaa malaika pamoja na magari ya vita yenye moto kumzunguka na kumlinda Elisha!

Wewe unalo jeshi la malaika wamekuzunguka sasahivi,wanakulinda. Malaika wanatenda kazi juu ya neno la Mungu.Kila siku ni lazima uendelee kujenga polisi kwenye mji wako kwa kuongea, "Nimezungukwa na malaika wengi sasahivi!" Unapofanya hivi, malaika wataendelea kupigana na maadui, halisi au wa rohoni. Unapokuwa hauwezi kulala kwenye giza, mara zote kumbuka unayo magari ya vita makubwa na bora yenye moto yamekuzunguka. Kamwe usiogope kitu chochote, malaika wako wapo tayari kukulinda unapotamka neno.

## TAMKO LA KINABII

**I decree and declare that I am heavenly protected, I am surrounded by countless angels right now. Nothing can happen to me or my family in Jesus' name.**

**SOMO ZAIDI :** Waebrania 12:22



**1 Wakorintho 15:6**
**"Baada ya hayo,Yesu alionekana kwa waumini zaidi ya 500 kwa muda huo huo..."**

Watoto,jinsi gani treni ni bigijii? Yote huenda "chew,chew!"

Kama Mji unahakikisha kuna magari, mabasi, treni, na ndege za angani kwaajili ya watu kufika mahali. Unao mfumo wako mwenyewe wa usafiri ndani yako.

Watoto, angalia andiko letu hapo juu kwa umakini. Linasema wakati Yesu amefufuka kutoka kwenye kifo, alijitokeza kwa watu 500 wote walikuwa sehemu tofauti tofauti kwa wakati mmoja! Hebu fikiria unaongea na rafikiyako shuleni, na unaongea na kaka yako nyumbani wote kwa wakati mmoja! Unaweza vipi kuwa sehemu mbili tofauti kwa wakati mmoja? Vizuri, Yesu alikuwa sehemu 500 tofauti kwa wakati mmoja! Unaweza kufanya yote aliyofanya Yesu na makubwa zaidi! Inawezekana kwako kama tu UTAAMINI! Hautachelewa kamwe shuleni tena! Hauhitaji kuwa kama binadamu wengine kutumia usafiri na magari. Tumia nguvu ndani yako.

## TAMKO LA KINABII

**Nina kiri na kutamka ninaweza kuwa sehemu nyingi kwa wakati mmoja,Kama vile Yesu.Nina weza yote katika Kristo! Haleluya!**

**SOMO ZAIDI**
Matendo 8:39-40



**Yuda 1:20**
**"Lakini rafiki zangu wapendwa,tumieni imani yenu takatifu kujijenga wenyewe zaidi kwa nguvu. Omba pamoja na Roho mtakatifu."**

Tulikuwa na wiki yenye shughuli nyingi ya kujenga Mji kwa kuongea neno la Mungu. Sasa Tutaangalia jinsi gani ya kujenga kwa kuomba katika Roho mtakatifu. Umeona sasa unalo neno la Mungu katika kila eneo la Mji wako,unaweza kuimarisha Mji wako, kwa kuomba katika Roho Mtakatifu.

Unakumbuka wale nguruwe wadogo watatu? Mmoja alijenga nyumba kwa mrija na mmbwa mwitu alipuliza mbali kwasababu haikuwa na nguvu. Mwingine alijenga kwa mbao na bado haikuwa imara. Kwahiyo, Nguruwe wote walikimbilia kwenye nyumba iliyojengwa imara kwa matofali, na mmbwa mwitu waliguna na kujivuna lakini bado hawakuw eza kuipeperusha mbali.

Mmeona watoto, unapoomba kwa kunena kwa lugha ya Roho mtakatifu na kutumia maneno uliyojifunza wiki hii. Adui ataguna na kujivuna na pia atachoka atakimbia mbali kwasababu Mji wako una nguvu. Amina!

## TAMKO LA KINABII

**Ninapoomba kwa lugha ya Roho mtakatifu, Mji wangu unakuwa imara. Kamwe sitoshindwa katika jina lenye nguvu la Yesu. Amina!**

**SOMO ZAIDI :** Luka 6:48 ICB



**3 Yohana 1:2**
**"Rafiki yangu mpendwa,Najua nafsi yako inaendelea vizuri. Ninaomba kwamba uendelee vizuri katika kila eneo na pia kwamba afya yako ni nzuri".**

Ulishawahi kuumwa,au kuwa na maumivu yasiyo acha? Labda kama upo hospitali kumuona daktari aliyekuambia uendelee kumeza dawa zenye ladha mbaya. Wakati mwingine unaweza kujiskia maumivu makali na kufikiri Mungu hayupo nawewe kukupa uponyaji. Unaweza hata kumuuliza Mungu kwanini unaendelea kujiskia kuumwa.

Vizuri,nina Habari njema kwenu watoto. Andiko letu la leo linatuambia kwamba Mungu kamwe hataki kutuona tukiumwa au kuwa na maumivu. Amekupa wewe maisha yake Kwahiyo hauwezi kuumwa kama watoto wengine shuleni. Wewe ni wa tofauti; wewe ni wa kipekee sana na umebeba afya ndani yako. Sio tu afya ya kikawaida lakini afya kama ya Mungu!kama Mungu anataka uwe na afya, magonjwa au maumivu hayaruhusiwi kuwa kwenye mwili wako, Kwahiyo kataa maumivu na amuru afya ya kimungu kwenye mwili wako sasa.

## TAMKO LA KINABII

Nina kiri na kutamka kwamba mimi ni wa kipekee,Sitokuja kuumwa. Nina afya,na ninakataa maumivu yeyote au magonjwa ndani ya mwili wangu katika jina la Yesu.

**SOMO ZAIDI**
Yeremia 33:6 ICB



**Marko 2:9**
**"Kipi ni rahisi:kumwambia huyu mtu aliyepooza,Dhambi zako zimesamehewa,' au kumuambia Simama juu chukua mkeka wako na utembee?"**

Ulishawahi kuwa kwenye hospitali ambapo watu na watoto wanaumwa? Baadhi ya watu, inaweza kuwa sehemu inayotisha kwasababu ya mashine zote na ma daktari wakisema maneno makubwa usiyoyaelewa. Wakati mwingine hii inaweza kukufanya ufikiri kwamba kumponya mtu ni vigumu sana na ni kwaajili ya watu wazima. Ninayo Habari njema kwako! Inaweza kuwa ni vigumu kwa ma daktari kumponya kipofu au kuwafanya wale wanaotembelea viti vya matairi lakini sio kwa Mungu.

Kwenye andiko letu leo, Yesu ametudokeza kwamba kwakwe,uponyaji ni rahisi. Ni rahisi sana. Unachotakiwa kufanya ni:

A:Tafuta neno kuhusu uponyaji na ulikubali
B:Amini katika hilo neno
C:Tamka hilo neno A.B.C!

Ukifanya hivi kwa kuendelea, magonjwa yatatoweka.
Kumbuka, lazima uliamini neno linalosema kuhusu uponyaji.

## TAMKO LA KINABII

**Ninatamka uponyaji juu ya maisha yangu na maisha ya familia yangu. Afya njema ni fungu langu katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI:** Isaya 53:4



**Warumi 8:10**
**"Mwili wako utakufa mara kwa mara kwasababu ya dhambi.Lakini kama Yesu yupo ndani yako,basi Roho atakupa uhai kwasababu Kristo amekufanya sawa pamoja na Mungu ".**

Je, unayo simu ya mkononi au umemuona mtu mzima anayo? Umeshawahi kugundua kuna muda,wanaiweka mahali kuchaji? Umeona, betri za simu za mkononi zinaisha chaji. Kama hauto zichaji, zitazimika moja kwa moja.

Maisha yako yanafanana na hii. Hata kama umezaliwa tena, muda mwingine mwili wako ni dhaifu, unajiskia maumivu au ugonjwa, na una hitaji kukaa kitandani. Andiko letu leo linasema kwamba kama Kristo yupo ndani yako, basi Roho anakupa uhai kwenye mwili wako au nguvu ya kuwa vizuri tena kwasababu upo Sawa pamoja na Mungu. Asifiwe Yesu!

Hautakiwi kumfanya Roho akupe uhai, Tayari ameshafanya hivyo.unaweza ukawa bado unasikia maumivu lakini endelea kutamka kwamba Roho mtakatifu anaendelea kukupa uhai kila mara na maumivu yatapotea. Endelea kusema na usiache!

## TAMKO LA KINABII

Roho mtakatifu ananipa uhai katika mwili wangu kwasababu Nipo sawa pamoja na Mungu. Ninakataa magonjwa na maumivu katika jina la Yesu.

**SOMO ZAIDI :** Warumi 8:10-11



**Yohana 10:10**
**"Mwizi anakuja kuiba na kuua na kuharibu.Lakini nilikuja kuwapa uhai—uhai katika ukamilifu wake wote."**

Ni andiko la kushangaza leo! Yesu alikuwa akisema kwamba alikuja kukupa wewe uhai, uhai katika ukamilifu wake wote Haleluya kwa Mungu! Watoto, maisha yako sio kama ya rafiki zako shuleni au watu unaowaona wanaokuzunguka. Hao watu wanaenda kwa daktari pale wanaooumwa; wanaenda benki kama wanahitaji pesa, na kuendelea. Lakini wewe ni kiumbe tofauti.

Umeona, uhai aliokupa Yesu sio uhai wa mwanadamu. Supamani ana uhai wa alieni lakini wewe unao uhai Sawa na wa Mungu. Uhai sawa Sawa kama wa Mungu. Haleluya! Uhai wa Mungu umekamilika maana hakuna ugonjwa au kifo ndani yake. Kamwe usikubali magonjwa au maumivu ndani ya mwili wako au kwenye familia yako. Wakati huo unaona, amuru yaondoke katika jina la Yesu' na tamka uponyaji uchukue nafasi!

## TAMKO LA KINABII

Nina uhai uliokamilika.Nina maisha ya Mungu ndani yangu;kwahiyo Nina amuru magonjwa yote na maumivu kutoka nje!Asante,Yesu!

**SOMO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:17



**Waebrania 10:14**
**"Maana kwa sadaka moja amewakamilisha hata milele wale waliofanywa wa takatifu."**

Watoto, hivi unajua ya kwamba unapojihisi maumivu, au kuugua ni kweli unajiskia maumivu au kuumwa? Ngoja niwaonyeshe.

Andiko letu la leo linatuambia kwamba roho tuliopewa ni mkamilifu. Hana mtiririko, hana madhaifu/mapungufu. hachoki wala kuumwa. Jambo la ukweli, roho yako hailali. ni mwili wako unapata udhaifu, uchovu, na ugonjwa, na usingizi. Mwili wako ndio unajiskia maumivu,lakini wewe sio mwili wako. Wewe ni roho. Kwahiyo ukiumwa kichwa, unasema mwili wangu unaumwa kichwa, sio mimi! Mwili wako ni nyumba ya roho.

Kwahiyo unawezaje kujiondoa kwenye maumivu? Mwili wako unasikiliza maneno yako. Ongea afya kwenye mwili wako, na mwili wako utasikiliza. Kumbuka watoto, Roho mtakatifu ndani yako anakupa uhai.


## TAMKO LA KINABII

**Nina tamka uzima na afya njema kwenye mwili wangu sasahivi katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI**
Warumi 8:9

# My goodnews notes

# Hello kids can you find these 10 objects in the picture?





Marko 11:23
"Nina waambia ukweli.Unaweza kusema na mlima huu, Nenda, mlima anguka baharini. 'Na kama hauna wasiwasi katika akilizako na ukaamini ulichosema kitatokea, basi Mungu atafanya kwaajili yako."

Watoto, milima inawezaje kuona? Ni rahisi, inaongea! Andiko letu la leo ni Yesu anatuambia kwamba tunaweza kuongea na milima! Milima anayoongelea ni matatizo kwenye maisha yako ambayo yanaonekana kuwa makubwa kuyatatua. Unaweza kuongea na huo mlima na kuuambia nn chakufanya. Kwa mfano,Kama kuna ugonjwa au maumivu mwilini mwako au kakayako na dadayako, unaweza kuongea na mlima huo na kuuambia utoke au ukatupwe ndani ya bahari, na itakuwa!unatakiwa uamini kwamba utakachosema kitakuwa.

Mllima wowote unaokutana nao, Kama ni afya, huzuni, au hofu, ongea nao kama Yesu na uuambie nini unataka ufanye.

## TAMKO LA KINABII

Nina tamka kwa kila mlima kwenye maisha yangu upigwe chini.Nina ongea na kila ugonjwa, huzuni, na hofu ndani ya maisha yangu yapotee katika jina la Yesu.

**SOMO ZAIDI**
Marko 11:12-24 ICB



**Methali 17:22**
**"Moyo wenye furaha ni kama dawa nzuri.Lakini roho iliyovunjika hukausha mifupa."**

Madaktari huwapa wagonjwa dawa kuwasaidia kupona.Wakati mwingine zinakuwa na ladha mbaya sana, na baadhi ya watu wanatumia kilasiku au maranyingi kwa siku. Labda kama ulishawahi kuwa na dawa zenye ladha mbaya pia. Lakini unajua kwamba Mungu anazo dawa kwaajili ya watoto wake? Hebu tuangalie andiko letu la leo kwa umakini zaidi.

Moyo wa furaha ni kama dawa nzuri kwako.Kamwe hauwezi kuumwa kama ukichagua kuwa na furaha na shangwe. Shangwe zina weka mbali magonjwa. Kwahiyo unapokuwa unaianza siku yako, shangilia hata kama kila kitu kinacho kuzunguka kinakupa huzuni. Kuwa na huzuni, hasira, na uchungu vitakukausha nguvu zako tuna kusababisha ujiskie kuumwa. Furaha ya Mungu ni nguvu zako. Haleluya. Hiyo ndio dawa yako.

## TAMKO LA KINABII

**Leo,ninachagua furaha hata itokee nini kunako nizunguka. Ninakataa kukwazika, hasira au kiburi. Nina chagua furaha katika jina la Yesu**

**SOMO ZAIDI**
Nehemia 8:10



**Yohana 17:16**
**"Wao sio wa ulimwengu huu,Kama mimi pia sio wa ulimwengu."**

Bwana Yesu alikuwa anatuombea kabla Hajasulubiwa hapo aliposema kwenye andiko letu la leo.

Ukweli ni kwamba wewe sio binadamu kama watu wengine wanao kuzunguka. Unaweza kufanana kama wao, na kuongozana nao,lakini hawawezi kufanya vitu kama unavyo fanya wewe. Unapo mpokea Yesu kama Bwana, hautoi maisha yako kwa Yesu kubadili. Yesu anayatupa maisha yako ya zamani na anakupa maisha yake mwenyewe!Haleluya!Maisha yasiyo ya kawaida na ya kawaida ya Mungu!

Umeona, unapoomba, vitu vinabadilika. Wakati binadamu maranyingi wanatembea katika chuki, maumivu na huzuni, wewe kwa mfululizo unatembea ndani ya upendo na furaha. Hayo ndio aina ya maisha ya Mungu. Mara zote kumbuka, Umezaliwa na Mungu na wewe ni mshindi.

## TAMKO LA KINABII

**Nina kiri na kutamka kwamba mimi sio binadamu. Mimi ni Mungu, mtoto wa aliye juu sana. Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo! Haleluya!**

**SOMO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:17



**Yohana 10:34**
**Yesu akajibu, "imeandikwa kwenye sheria zenu kwamba Mungu kasema, 'Nimesema ninyi ni miungu!"**

Kama mmbwa wanazaa mmbwa,-binadamu wanajifungua binadamu,na mbuzi wanazaa mbuzi, lakini Mungu anamzaa nani? Wewe otea, mungu! Wewe ni mtoto wa Mungu na hiko ndio kinakufanya uwe mungu, sio binadamu!Yote hayo kwasababu ya Yesu. Je, unajua kwanini? Ngoja nikuonyeshe.

Biblia inasema kuingia kwa neno la Mungu kunaleta mwanga (nuru) (Zaburi 119:130 NKJV). Hii inamaanisha kila muda unasikiliza mafundisho kanisani au kusoma biblia au (GoodNews Daily), mwanga unaingia ndani yako.Lakini kumbuka, Mungu ni nuru, kwahiyo unaweza kusema kuingia kwa neno la Mungu kuna mleta Mungu. Kadiri unaposoma kuhusu au kusikiliza kuhusu neno la Mungu, ndivyo kadiri unafanana nae kama Mungu, Wewe ni mungu.

## TAMKO LA KINABII

**Nina kiri na kutamka kwamba nimezaliwa na Mungu na, pia ni mungu. ninaishi maisha kama ya Mungu na kuleta matokeo ya kimungu katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI**
Zaburi 119:130



**Waefeso 5:30**
**"Sisi ni sehemu ya mwili wake,nyama zake na mifupa yake."**

Hivi unajua kwamba wewe sio mfuasi wa Kristo?Kuwa mkristo haimaanishi unamfuata Yesu. Unawezaje kuwa mfuasi wakati wewe ni sehemu ya viungo vya mwili wa Yesu?

Yesu hana mwili hapa duniani; Mwili wake umeenda mbinguni. Halafu pia akamtuma Roho mtakatifu aje kuishi duniani,lakini kulikuwa na tatizo. Roho anahitaji mwili aweze kuishi ndani ili aweze kufanya kazi. Mwili pekee Roho mtakatifu anaweza kuutumia ni wako! Unaupamba mwili wake. Kwahiyo, haumfuati Yesu kwasababu Roho yumo ndani yako. Ni kama kusema tumbo au miguu inakufuata, na wakati ni sehemu ya mwili wako!

Vivyo hivyo,Wewe ni sehemu ya viungo vya Yesu'. Hii inamaanisha unaposogeza kichwa chako,unasogeza vidole, au kuongea, ni Yesu afanyaye hayo.

## TAMKO LA KINABII

**Mimi ni Viungo vya mwili vya Kristo. Ninapoongea, Yesu anaongea. Ninapotembea!ninapo omba, Yesu anaomba! Kristo ndani yangu tumaini la Utukufu. Haleluya!**

**SOMO ZAIDI**
Waefeso 5:1



Marko 3:17
"Yakobo na Yohana,wana Zebedayo (Yesu aliwapa majina Boanegazi,(Boanerges)ambayo maana yake "Wana wa radi");"

Umeshawahi kusikia mlio mkubwa,mngurumo wa radi wakati mvua inanyesha? Kwa watu wengi, pamoja na wakubwa, inatisha, na watoto hujificha kwenye ma blangeti yao! Mawingu meusi hujikusanya na miale ya mwanga huja kuangaza kabla ya mlio wa radi. Hivi unajua kama mwana wa Mungu, kamwe hutakiwi kuiogopa?

Umeona, unayo radi ndani yako tena yenye sauti kubwa, na dunia nzima inasubiri kuona na kusikia nini utafanya nayo. Lakini kabla ya dunia kuisikia radi yako, lazima kuwe na mwanga kwanza. Tumejifunza hapo nyuma kwamba neno la Mungu linaleta mwanga. Kadiri unavyo soma na kulisikia neno la Mungu, ndivyo kadiri mwanga ndani yako na sauti kubwa ya radi ndani yako itasikika. Unaweza kuonekana mdogo lakini ukiomba, ukifanya kama neno la Mungu linavyosema, wewe ni zaidi ya radi unayoisikia kwenye mawingu.

## TAMKO LA KINABII

Mimi ni mwana wa radi,na dunia yote inanisubiri mimi niwaonyeshe nguvu ya Mungu katika jina la Yesu. Haleluya!

SOMO ZAIDI
Warumi 8:22



**Yohana 4:24**
**"Mungu ni roho. Wao wanao muabudu Mungu lazima wamuabudu katika roho na ukweli"**

Kwa wewe mtoto wa Mungu, inakufanya wewe uwe roho na sio mwanadamu. Kitu pekee ambacho roho yako imekufanya mwili wako kuwa nyumba yake. Hivi unajua roho yako inafikiri tofauti na mwili wako? Roho yako inafikiri Sawa Sawa kama Mungu afanyavyo, lakini mwili wako una mawazo yake. Kwa mfano, wakati mwingine unajisikia huzuni sana kuhusu wewe mwenyewe na kuanza kusema vitu kama "Siwezi kufanya hivi", " Mimi sio mwerevu", " Hakuna mtu ananipenda", Ninajiskia kuumwa", na kuendelea.

Roho yako mara zote inayo furaha, Kama Mungu. Roho yako inataka kuomba, kwenda kanisani, kuwa mkarimu kwa wengine, na uwe na afya.

Ukifanya Kama roho yako inavyotaka, unatembea katika mtikisiko ule ule kama Mungu. Lisha zaidi roho yako kwa kusoma neno la Mungu mara kwa mara, na utaanza kutembea katika roho zaidi na zaidi. Kabla hujajua, Mungu ataanza kukuonyesha vitu kuhusu maisha yako na utakuwa unaweza kuwasiliana naye!

## TAMKO LA KINABII

**Ninatembea katika mtikisiko ule ule kama Mungu.Ninaongea roho na uhai muda wote. Mimic ni roho katika jina la Yesu!**

**SOMO ZAIDI:** Warumi 8:5-6



**Waebrania 12:22**
**"Lakini umetokea Mlima Sayuni kwenye mji wa Mungu anayeishi, Mbinguni Yerusalemu. Umekuwa maelfu na maelfu juu ya kundi la malaika wenye furaha."**

Mtoto wa Mungu, pindi umempokea Yesu Kristo, anuani yako hubadilika. Kama mtu akimuuliza Mungu Upo wapi sasa hivi, Mungu atajibu mlima sayuni. Unaweza usihisi, au kuona, lakini upo pale. hata Kama upo ndani ya blangeti sasahivi, shuleni, mtaani, Mungu anasema upo Mlima Sayuni!

Kutoka mahali hapa, unaweza kubadili maisha yako halisi kuwa kitu chochote unachotaka. Unachotakiwa kufanya ni kuongea lugha ya Sayuni. Kwa mfano, katika Isaya 33:24 (MSG) "Hakuna yeyote katika Sayuni, 'Atasema nina umwa.'", kwasababu hakuna ugonjwa Sayuni!

Mwili wako unaumwa sio wewe halisi, roho yako! Haleluya! Hata kama mwili wako unakuambia unaumwa sema "Nina afya!"

## TAMKO LA KINABII

**Nina afya,Mimi ni tajiri,na nina nguvu kwasababu mimi ni raia wa Mlima Sayuni katika jina la Yesu.Mimi sio ambavyo mwili unaniambia mimi nilivyo, Mimi ni kama Mungu anavyo sema!**

**SOMO ZAIDI:** Waebrania 12:22



HABARI NJEMA KILA SIKU KWA WATOTO



**Wakolosai 1:19**
**"Mungu ilimpendeza yeye kuishi katika Kristo."**

Mungu alifurahi sana kuwa na utimilifu wake ndani ya Kristo. Sasa Kristo anaishi ndani yako!Haleluya!

Tazama hii, mwili wako na nyumba ya Mungu! Kama watu waki kuuliza, "Mungu anaishi wapi?", wajibu "Anaishi ndani yangu!" Mtoto wa Mungu, humfuati Mungu lakini umembeba Mungu. Atukuzwe Yesu! Mungu alitafuta kote kuangalia mwili wa kuishi lakini hakuridhishwa mpaka alipokupata wewe. Wewe ulikuwa sahihi kwake.

Hii ina maana kwamba wewe ni makao makuu ya Mungu. Upo mahali Mungu anapanga mipango yake na kuandaa kuleta mabadiliko katika dunia. Atukuzwe Yesu. Kamwe usizungumze kinyume kuhusu wewe mwenyewe kwasababu wewe ni makao makuu ya Mungu. Kamwe usijione wewe ni wa chini zaidi ya mwingine. Jikumbushe mwenyewe umemmbeba Mungu ambaye aliiumba dunia.

## TAMKO LA KINABII

**Mimi ni makao makuu ya Mungu. Kristo ndani yangu tumaini la utukufu. Haleluya!**

**SOMO ZAIDI**
1 Wakorintho 6:19



**2 Wakorintho 5:20**
**"Sasa tena tumekuwa mabalozi wa Kristo..."**

Fikiria kumekuwa na sherehe iliyo andaliwa kwaajili yako. Wageni wote walialikwa, lakini unapofika, hakuna mgeni yeyote anayekufahamu! Hawakutambui na wanafikiri wewe ni mgeni tu mwingine, Hata hivyo ni sherehe yako.

Vizuri, watoto, Yesu anarudi hivi karibuni tena. Kabla Yesu hajarudi, Anataka tuwe tumeshavuna nafsi nyingi kwa Kristo. Vinginevyo, atakapokuja, hawatoweza kumtambua. Hivi unajua kwamba wewe ni balozi wa Kristo? Balozi ni mtu aliyetumwa na kiongozi wa nchi ili kumuwakilisha yeye kwenye nchi nyingine. Balozi huzungumza na viongozi wa nchi nyingine kuhusu nchi yake.

Nchi yako ni Mlima Sayuni, na dunia unayoiona ni nchi nyingine. Kazi yako ni kuwaambia watu wengi kadiri uwezavyo kuhusu Mungu na jinsi anavyo wapenda na anawataka waje kwake.

Muambie mtu leo kuhusu Yesu!

## TAMKO LA KINABII

**Nina kiri na kutamka mimi ni Balozi wa Kristo; Ninaongea kwa niaba ya Kristo. Nina wakilisha Mlima Sayuni katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI:** Waefeso 2:6



**2 Wakorintho 4:13**
**"Imeandikwa kwenye maandiko, "Niliamini, kwahiyo niliongea." Imani yetu ni kama hii, pia. Tunaamini, na kwahiyo tunaongea."**

Hivi unajua kama Mtoto wa mfalme, hutakiwi kuomba kwaajili ya pesa? Amini kwamba wewe ni tajiri na hupungukiwi kitu. Labda unafikiri wewe ni mdogo sana kuwa tajiri au huoni utajiri nyumbani au kwenye familia.

Kama mtoto wa Mungu, unatembea kwa imani, sio kwa unachokiona au kujiskia. Katika Mlima Sayuni, wewe huzeeki na ni tajiri wa pesa nyingi. Unaweza kusema kwa utajiri huo sasahivi ili wewe na familia yako muone. Andiko letu linasema lazima uamini wewe ni tajiri na uendelee kutamka kuhusu hilo. Umeona, ukiongea kuhusu utajiri, maneno yako yanatengeneza barabara ana daraja kwa malaika kuleta utajiri kwako hapa duniani.

Kama hamna vya kutosha kwenye familia yenu, basi tamka na useme, "Pesa zinakuja!" Kwa kurudia rudia. Utaziona pesa ziki miminika kwenu zaidi ya zamani!

## TAMKO LA KINABII

**Pesa zinanipenda mimi, pesa zinanifuata kila ninakokwenda, na mimi ni tajiri kupita kipimo. Pesa zinakuja! Haleluya!**

**SOMO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:7



**2 Wakorintho 9:7**
**"Kila mmoja hutoa, tena kile ambacho ameamua moyoni mwake kutoa. Hatakiwi kutoa kama inamfanya kuwa na huzuni. Na hatakiwi kutoa kama anafikiria amelazimishwa kutoa. Mungu anapendezwa na mtu anaye toa kwa kufurahia."**

Mungu anapenda kutoa. Kiukweli, Anapenda sana kutoa ndio maana akamtoa mwanae wa pekee kwetu, Yesu Kristo. Kwakuwa una Roho wa Mungu ndani yako,unayo pia roho ile ile ya utoaji. Kuna njia nyingi unaweza kutoa. Labda unazo pesa na unataka kutoa kanisani kusaidia kutangaza habari njema duniani kote. Labda kutabasamu kwa mtu anayeonekana na huzuni au kuzungumza naye anayeonekana mpweke. Hata kumkumbatia mtu au kumfariji mtu ni njia ya utoaji. Zote hizi ni njia za utoaji.

Kwahiyo, unapo tabasamu, kuongea au kutoa, huyo ni Roho mtakatifu anafanya kwasababu Kristo yupo ndani yako. Hii ni njia sahihi ya kusambaza habari njema kwasababu watu watajua kwamba Mungu anawapenda na anajali kuhusu wao kupitia wewe. Kuwa mtoaji kuanzia leo na ufanye hivyo ukifurahia!

## TAMKO LA KINABII

**Mimi ni mtoaji mwenye furaha. Ninapo Toa, Ninaonyesha habari njema kwa kilamtu. Kila mahali ninapo kwenda,Nina Toa katika jina la Yesu.**

**SOMO ZAIDI:** 2 Wakorintho 9:7-8

# My goodnews notes


Would you like to share your testimony with us?
We would LOVE to hear from you children!
Write to us here:
kids@goodnewsworld.com


TheGoodNewsWorld Helplines
USA: +1 (240) 781-6942
UK: +44 333 344 8612
RSA: +27 (51) 004-0209
www.goodnewsworld.com